# HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

**1.9.2015**

**Kumb. KGR/MSY/C.4/46**

**KWA WANANCHI WOTE**
**TANZANIA BARA**

**YAH: TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI WA TAKA NGUMU (SOLID WASTE)**

Halmashauri ya Wilaya Missenyi inakaribisha maombi toka kweye Taasisi binafsi, Kampuni , Mashirika mbalimbali, Vikundi mbalimbali na Watu wenye uwezo kwa ajili ya kukusanya taka ngumu( solid waste) katika miji ya Mutukula,Bunazi na Kyaka kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1.10.2015 hadi tarehe 30.6.2016

MASHARTI KWA MUOMBAJI

1) Awe mtu mzima na mwenye akili timamu mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
2) Muombaji a ambatanishe nakala ya usajili wa Kampuni yake pamoja na TIN
3) Muombaji aambatanishe mchanganuo kuonesha jinsi atakavyofanya kazi yake kwa ufanisi.
4) Stakabadhi za kukusanyia mapato zitanunuliwa kwenye Hazina ya Halmashauri,pia vibutu vyote vitarejeshwa kwenye Hazina ya Halmashauri kwa ajili ya kutunzwa.
5) Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi au Taasisi yoyote ya Kiserikali.

8.Ada ya Maombi ni 50,000/= ambazo hazitarudishwa(Non-refundable fee) na risiti ya kulipia iambatanishwe na zabuni atakayoomba. Halmashauri haitapokea hundi au`money fax

6) Viwango vya kutoza kwa kila kaya ni shs 2000.00 kwa Mwezi, Maduka, Kioski na Viwanda Vidogo ni shs .4000.00 kwa Mwezi na Viwanda Vikubwa, Hoteli na taasisi ni shs Tshs 5000.00 kwa Mwezi.
7) Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ndiyo mwamuzi wa mwisho,hivyo ina uwezo wa kukataa au kukubali Zabuni kwa kuzingatia Sheria,Kanuni na taratibu zilizowekwa bila kujali bei ya juu au ya chini bali takwimu zenye viwango halisi zitazingatiwa.

8) Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe 22.9.2015 saa 8.00 mchana na Zabuni zote zitafunguliwa siku hiyo hiyo saa 8.30 mchana. Waombaji au wawakilishi wa Makampuni wanaombwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni.Fika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.
9) Zabuni zote zifungwe kwa lakiri na bahasha juu iandikwe kwa herufi kubwa zabuni iliyoombwa na zitumwe kwa;
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI**
**S.L.P 38,**
**KYAKA**
**MISSENYI.**

ELIZABETH S. KITUNDU
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI**

NAKALA: KATIBU TAWALA (M) KAGERA

KATIBU TAWALA (W) MISSENYI

HALMASHAURI ZOTE ZA (W) ZA MKOA WA KAGERA

MANISPAA YA MKOA WA KAGERA

Mbao zote za Matangazo .
**MISSENYI**